

**KILA JARIBU ANALOKUTANA NALO MWANA WA MUNGU**  
**LINA MAJIBU (UTATUZI WAKE) MBELE ZA MUNGU**  
**MAANDIKO: 1KOR. 10:13**

**1. UTANGULIZI:**

Ni kweli kabisa kwamba jaribu la aina yoyote halifurahishi, lakini ni ukweli usiokanushika kwamba kila mtu lazima tu atakutana na majaribu hata kama ni tajiri sana au maskini sana; aliyeoa au asiyoa, aliyeolewa au asiyeolewa; aliye na biashara ndogo au kubwa n.k.

**2. Kuna aina tatu (vyanzo vitatu vya majaribu)**

**a. Kuna majaribu ambayo chanzo chake ni Mungu mwenyewe (Mungu anatoa mtihani) kwa mtoto wake ampendaye. Mwz. 22: 1 – 2.**

- Kabla ya urafiki wa Ibrahimu na Mungu haujaimarika, Mungu alimjaribu Ibrahimu.
- Hakuna mwanafunzi yeyote anayependwa na mwalimu wake kwa dhati ambaye atapanda madarasa bila kupewa mitihani ya kufanya
- Majaribu yanayotokana na Mungu Yakobo anasema kwamba tunatakiwa kuyafurahia kwa sababu lengo lake ni kutupima ili tunapoyashinda tupate kuingia katika daraja lingine- **Yako.1 : 2 – 4, 1Pet. 5 -7**; Majaribu yanayotokana (ambayo chanzo chake ni Mungu yana heri mbele zake. **Yak. 1:12.**

**Note: Majaribu yanayotoka kwa Mungu lengo lake kubwa ni kutaka kuujua moyo wa mtu ukoje ukilinganisha na vitu alivyonavyo. Mark. 10: 17 – 23**

**b. Kuna majaribu mengine ambayo chanzo chake ni shetani mwenyewe. Yak. 1: 13 – 15**

- Mtu yeyote ambaye hayuko upande wa ibilisi yeye ibilisi atafanya juu chini kwa kuleta majaribu

mbalimbali kwake lengo kubwa likiwa ni kutaka kumfanya huyo mtu afanye dhambi kama alivyofanya kwa Ayubu – **Ayub. 1: 8 – 22, Ayub. 2: 1 – 10**; alifanya kwa Yusufu, kwa Daniel nk.

**Note: Walio upande wake ibilisi daima haangaiki nao.**

- Hata Yusufu alipokuwa anajaribiwa na mke wa Potifa, haya hayakuwa majaribu yanayotoka kwa Mungu kutokana na malengo yake; majaribu yoyote ambayo yanalenga utende dhambi, haya hayatoki kwa Mungu bali kwa yule mwovu.
- **Narudia kusema kwa mkazo kwamba majaribu yanayotokana na Mungu hayana lengo kabisa la kumfanya mtu atende dhambi bali kuujua kwa kina moyo wake. Kut. 20:20, Kumb. 8: 1 – 2, Mar. 10: 17 – 23.**
- c. **Majaribu aina ya tatu ni yale ambayo chanzo chake ni mtu mwenyewe, yaani ni majaribu ambayo yanasababishwa na mtu mwenyewe. 2Samwl. 11: 1 – 4.**
  - Aina hii ya majaribu haifurahishi hata kidogo maana inaleta hasara kubwa. Jaribu alilolanzisha Mfalme Daudi mwenyewe sote tunalifahamu lilivyomgharimu sana hadi kuja kupata ushindi baadae.
  - Jaribu hili huwapata wote wanaofanikiwa, na kisha wanaamua kustarehe!!!
  - Kitendo cha Daudi kukataa kwenda vitani na kutuma mwingine amwakilishe kilikuwa ni kinyume kabisa cha sheria ya Wafalme saa ya vita; yeye ndiye aliyetakiwa kutoa amri pamoja na maelekezo mengine; yeye ndiye mkubwa wa majeshi, halafu anabaki amestarehe na wakati huo huo askari wadogo wanapigana vita na kuuawa!! **Kuanzisha jaribu baada ya kufanikiwa ni jambo la hatari sana; afadhali jaribu liletwe na Mungu kuliko kujiletea jaribu wewe mwenyewe.**

- Jaribu hili mara nyingi halina mlango wa kutokea; na kutoka katika jaribu ambalo chanzo chake ni wewe mwenyewe lazima tu utalipa gharama.

**Mfano:** Kijana ambaye anaamua kuolewa na mtu ambaye hajaokoka (**2Wak. 6: 14 – 18**) **itakugharimu!! Mfano** wa **Mwalyego** (kuwa na imani iliyopilitiza na kuoa mlemavu kwa madai kwamba ... ili mgharimu kuacha wokovu!! Kijana **aliyefunga siku 40** ili awe kama Yesu ilimgharimu

3. Ni kweli kabisa kwamba changamoto mbalimbali tunazokutana nazo ndizo ngazi zinazobeba mafanikio yetu, na kwamba baraka zetu zote na ushindi wetu vyote vinabebwa na changamoto tunazopitia kila siku; lakini changamoto tunazozianzisha sisi wenyewe, kamwe kamwe siyo ngazi inayobeba baraka zetu, badala yake tutalipa gharama ya kutosha na bila neema ya Mungu inaweza kuwa ndiyo mwisho wa safari yetu nzuri ya kwenda kumlaki Mwokozi wetu Yesu!!. **Waam. 14: 1 – 3, 16: 1 – 5, 15 – 25**

“ Ee Bwana uniumbie moyo safi. Amina.

**Na**  
**Askofu Dr. L. Mwizarubi**  
**May 2021**